**القرآن الكريم كتاب رحمة للعالمين**

**KHUTBA YA KWANZA**

**Qurani Tukufu Kitabu cha rehma kwa walimwengu**

**Imefasiriwa**

**na**

**profesa / Ayman Alasar**

**Kitivo cha lugha na Ufasiri Alazhar**

Shukrani zote anastahiki Mwenyezi Mungu Mlezi wa walimwengu, Msemaji ndani ya Kitabu chake Kitukufu: وَنُنَزِّلُ مِنَ الْقُرْآنِ مَا هُوَ شِفَاءٌ وَرَحْمَةٌ لِلْمُؤْمِنِينَ {**Na tunateremsha ndani ya Qurani ponyo na rehma kwa Waumini**} na Mwenyezi Mungu Mtukufu Anasema: وَهَذَا كِتَابٌ أَنْزَلْنَاهُ مُبَارَكٌ فَاتَّبِعُوهُ وَاتَّقُوا لَعَلَّكُمْ تُرْحَمُونَ {**Na hiki Kitabu tumekiteremsha kimebarikiwa hivyo kifuateni na Muogopeni Mwenyezi Mungu mpate kuhurumiwa**}. Ninashuhudia kuwa hakuna mola wa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu peke yake hana mshirika, na ninashuhudia kuwa Mtume wetu Muhammad ni mja wake na Mtume wake. Ewe Mwenyezi Mungu peleka rehma na amani pamoja na baraka kwake na kwa watu wa nyumbani kwake na Maswahaba wake na kwa wale wote waliomfuata kwa wema mpaka siku ya malipo.

**Baada ya Utangulizi**:

Qurani Tukufu ni kamba imara ya Mwenyezi Mungu na ukumbusho wenye hekima, mwenye kuzungumza kwa Qurani amesema kweli, mwenye kuhukumu kwa Qurani atafanya uadilifu, na mwenye kushikamana nayo kitamuongoza kwenye njia iliyonyooka. Wanachuoni hawashibi nayo, wala kukatika maajabu yake, wala kufikwa na batili ndani yake wala nyuma yake, ambapo Mwenyezi Mungu Mtukufu Anasema:

إِنَّهُ لَقُرْآنٌ كَرِيمٌ * فِي كِتَابٍ مَكْنُونٍ * لَا يَمَسُّهُ إِلَّا الْمُطَهَّرُونَ * تَنْزِيلٌ مِنْ رَبِّ الْعَالَمِينَ.

{**Hakika hii bila ya shaka ni Qurani Tukufu * Katika Kitabu kilicho hifadhiwa * Hapana akigusaye ila walio takaswa * Ni uteremsho unao toka kwa Mola Mlezi wa walimwengu wote**}. Na Mola Mtukufu Anasema:

وَإِنَّهُ لَكِتَابٌ عَزِيزٌ * لَّا يَأْتِيهِ الْبَاطِلُ مِن بَيْنِ يَدَيْهِ وَلَا مِنْ خَلْفِهِ تَنزِيلٌ مِّنْ حَكِيمٍ حَمِيد.

{**Na haya bila ya shaka ni Kitabu chenye nguvu na utukufu * Hautakifikia upotovu mbele yake wala nyuma yake. Kimeteremshwa na Mwenye hekima, Msifiwa**}.

Qurani Tukufu ni Kitabu cha rehma kwa walimwengu, ambapo Mwenyezi Mungu Mtukufu Anasema:

يَا أَيُّهَا النَّاسُ قَدْ جَاءَتْكُمْ مَوْعِظَةٌ مِنْ رَبِّكُمْ وَشِفَاءٌ لِمَا فِي الصُّدُورِ وَهُدًى وَرَحْمَةٌ لِلْمُؤْمِنِينَ* قُلْ بِفَضْلِ اللهِ وَبِرَحْمَتِهِ فَبِذَلِكَ فَلْيَفْرَحُوا هُوَ خَيْرٌ مِمَّا يَجْمَعُونَ.

{**Enyi watu! Yamekujieni mawaidha kutoka kwa Mola wenu Mlezi, na poza kuponyesha yaliyomo vifuani, na uwongofu, na rehema kwa Waumini * Sema: Kwa fadhila ya Mwenyezi Mungu na rehema yake! Basi nawafurahi kwa hayo. Haya ni bora kuliko hayo wanayo yakusanya**}.

Na Mola Mtukufu Anasema: وَنزلْنَا عَلَيْكَ الْكِتَابَ تِبْيَانًا لِكُلِّ شَيْءٍ وَهُدًى وَرَحْمَةً وَبُشْرَى لِلْمُسْلِمِينَ {**Na tumekuteremshia Kitabu hiki kinacho bainisha kila kitu, na ni uwongofu, na rehema, na bishara kwa Waislamu**}. Na Anaendelea kusema:

تِلْكَ آيَاتُ الْكِتَابِ الْحَكِيمِ * هُدًى وَرَحْمَةً لِلْمُحْسِنِينَ.

{**Hizi ni Aya za Kitabu chenye hekima * Kuwa ni Uwongofu na Rehema kwa wafanyao wema**}. Mola Anasema tena:

وَلَقَدْ جِئْنَاهُمْ بِكِتَابٍ فَصَّلْنَاهُ عَلَى عِلْمٍ هُدًى وَرَحْمَةً لِقَوْمٍ يُؤْمِنُونَ.

{**Na hakika tumewaletea Kitabu tulicho kipambanua kwa elimu, uwongofu na rehema kwa watu wenye kuamini**}.

Mada ya rehma imekuja ndani ya Qurani Tukufu zaidi ya mara mia mbili, ambapo Qurani Tukufu imebainisha kuwa rehma sifa katika sifa za Mwenyezi Mungu Mtukufu. Mola Anasema: وَرَحمَتِي وَسِعَتْ كُلَّ شَيْءٍ {**Narehema yangu imeenea kila kitu**}. Na Mola Mtukufu Anasema: وَرَبُّكَ الغَنِيُّ ذُو الرَّحْمَةِ {**Na Mola wako Mlezi ndiye

**Mkwasi, Mwenye rehema**}. Na Anasema tena: وَرَحْمَتُ رَبِّكَ خَيْرٌ مِمَّا يَجْمَعُونَ {**Na rehema za Mwenyezi Mungu ni bora kuliko hayo wanayo yakusanya**}. Mola Ameendelea kusema: كَتَبَ رَبُّكُمْ عَلَى نَفْسِهِ الرَّحْمَةَ {**Mola wenu Mlezi amejilazimisha rehema**}.

Mwenye kuzingatia yaliyomo ndani ya Qurani Tukufu atafahamu rehma za Mwenyezi Mungu Mtukufu zipo kwa walimwengu, ambapo Mwenyezi Mungu Mtukufu Ameumba usiku na mchana ikiwa ni rehma kwa viumbe vyake vyote, ili wapate kupumzika usiku na kufanya kazi mchana ili kujipatia riziki na kujenga ulimwengu, kama vile Mwenyezi Mungu Mtukufu Ameteremsha mvua ni rehma kwa walimwengu, ambapo Mola Anasema:

وَمِنْ رَحْمَتِهِ جَعَلَ لَكُمُ اللَّيْلَ وَالنَّهَارَ لِتَسْكُنُوا فِيهِ وَلِتَبْتَغُوا مِنْ فَضْلِهِ وَلَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ.

{**Na ni katika rehema zake amekufanyieni usiku na mchana mpate kupumzika humo na mtafute fadhila zake, na ili mpate kushukuru**}. Na Mola Anasema tena:

وَهُوَ الَّذِي يُرْسِلُ الرِّيَاحَ بُشْرًا بَيْنَ يَدَيْ رَحْمَتِهِ حَتَّى إِذَا أَقَلَّتْ سَحَابًا ثِقَالًا سُقْنَاهُ لِبَلَدٍ مَيِّتٍ فَأَنْزَلْنَا بِهِ الْمَاءَ فَأَخْرَجْنَا بِهِ مِنْ كُلِّ الثَّمَرَاتِ كَذَلِكَ نُخْرِجُ الْمَوْتَى لَعَلَّكُمْ تَذَكَّرُونَ.

{**Na Yeye ndiye anaye peleka pepo (za kuvuma) kuwa ni bishara kabla ya kufika rehema yake. Hata hizo pepo zinapo beba mawingu mazito tunayachunga mpaka kwenye nchi iliyo kufa. Kisha tunateremsha kwayo maji, ndio kama hivyo tukatolesha kila aina ya matunda. Basi ndio hivyo hivyo tunavyo wafufua wafu, ili mpate kukumbuka**}.

Qurani Tukufu imebainisha kuwa Mola Mtukufu ameleta Mitume na akateremsha Vitabu kuwa ni rehma kwa walimwengu, ambapo Mola Mtukufu Anasema:

أَوْ تَقُولُوا لَوْ أَنَّا أُنْزِلَ عَلَيْنَا الْكِتَابُ لَكُنَّا أَهْدَى مِنْهُمْ فَقَدْ جَاءَكُمْ بَيِّنَةٌ مِنْ رَبِّكُمْ وَهُدًى وَرَحْمَةٌ.

{**Au mkasema: Lau kuwa tumeteremshiwa sisi Kitabu tungelikuwa waongofu zaidi kuliko wao. Basi imekufikieni bayana kutoka kwa Mola wenu Mlezi, na uwongofu, na rehema**}.

Mola Mtukufu Anasema kumuambia Mtume wake wa mwisho S.A.W:

وَمَا أَرْسَلْنَاكَ إِلَّا رَحْمَةً لِلْعَالَمِينَ.

{**Nasi hatukukutuma ila uwe ni Rehema kwa walimwengu wote**}.

Na Anasema tena:

لَقَدْ جَاءَكُمْ رَسُولٌ مِنْ أَنْفُسِكُمْ عَزِيزٌ عَلَيْهِ مَا عَنِتُّمْ حَرِيصٌ عَلَيْكُمْ بِالْمُؤْمِنِينَ رَءُوفٌ رَحِيمٌ.

{**Hakika amekwisha kujieni Mtume kutokana na nyinyi wenyewe; yanamhuzunisha yanayo kutabisheni; anakuhangaikieni sana. Kwa Waumini ni mpole na mwenye huruma**}.

Kama vile Mola Mtukufu alivyowalingania watu ndani ya Qurani Tukufu matumaini na matarajio kwenye rehma zake na akabainisha kuwa rehma zake zipo karibu zaidi na watu wema, ambapo Mola Mtukufu Anasema:

قُلْ يَا عِبَادِيَ الَّذِينَ أَسْرَفُوا عَلَى أَنْفُسِهِمْ لا تَقْنَطُوا مِنْ رَحْمَةِ اللهِ إِنَّ اللهَ يَغْفِرُ الذُّنُوبَ جَمِيعًا إِنَّهُ هُوَ الغَفُورُ الرَّحِيمُ.

{**Sema: Enyi waja wangu walio jidhulumu nafsi zao! Msikate tamaa na rehema ya Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu husamehe dhambi zote. Hakika Yeye ni Mwenye kusamehe, Mwenye kurehemu**}.

Na anaendelea kusema: إِنَّ رَحْمَتَ اللهِ قَرِيبٌ مِنَ المُحْسِنِينَ {**Hakika rehma za Mwenyezi Mungu zi karibu kwa watu wema**}.

## KHUTBA YA PILI.

Shukrani zote anastahiki Mwenyezi Mungu Mlezi wa viumbe, rehma na amani zimuendee Mtume wa mwisho naye ni Mtume Muhammad S.A.W pamoja na watu wa nyumbani kwake na Maswahaba wake wote.

Hakuna shaka kuwa Muumini ni ambaye hujipamba na maadili ya Qurani Tukufu ambayo Mwenyezi Mungu ameyateremsha kuwa rehma kwa walimwengu, na kufuata mwenendo wa Mtume S.A.W ambaye Mwenyezi Mungu amemleta kuwa ni rehma kwa walimwengu, ambapo Mtume wetu S.A.W anasema:

الرَّاحِمُونَ يَرْحَمُهُمْ الرَّحْمَنُ، ارْحَمُوا مَنْ فِي الْأَرْضِ يَرْحَمْكُمْ مَنْ فِي السَّمَاءِ.

"***Watu wenye huruma uhurumiwa na Mwenyezi Mungu, wahurumieni waliopo ardhini mtahurumiwa na waliopo mbinguni***". Na anasema tena S.A.W:

جَعَلَ اللَّهُ الرَّحْمَةَ مِائَةَ جُزْءٍ، فَأَمْسَكَ عِنْدَهُ تِسْعَةً وَتِسْعِينَ جُزْءًا وَأَنْزَلَ فِي الْأَرْضِ جُزْءًا وَاحِدًا؛ فَمِنْ ذَلِكَ الْجُزْءِ يَتَرَاحَمُ الْخَلْقُ، حَتَّى تَرْفَعَ الْفَرَسُ حَافِرَهَا عَنْ وَلَدِهَا خَشْيَةَ أَنْ تُصِيبَهُ.

"***Mwenyezi Mungu amefanya rehma kuwa na sehemu mia moja, sehemu tisini na tisa amezishikilia kwake na akateremsha ardhini sehemu moja tu, kupitia sehemu hiyo viumbe hufanyiwa huruma, mpaka farasi huinua kwato zake mbali na mtoto wake kwa kuhofia kumkanyaga***".

Na pindi ngamia alipoonesha upole na kutokwa na machozi mbele ya Mtume S.A.W ndipo Mtume S.A.W akauliza:

**لِمَنْ هَذَا الجَمَلُ؟ فجاء فتى من الأنصار فقال: لي، يا رسول الله، فقال له (صلى الله عليه وسلم): (أَفَلَا تَتَّقِي اللَّهَ فِي هَذِهِ الْبَهِيمَةِ الَّتِي مَلَّكَكَ اللَّهُ إِيَّاهَا؟ فَإِنَّهُ شَكَا إِلَيَّ أَنَّكَ تُجِيعُهُ وَتُدْئِبُهُ**

"***Ngamia huyu ni wa nani? Ndipo akaja kijana wa Ansar akasema: Ni wangu ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, Mtume S.A.W akasema kumuambia kijana: Hivi humuogopi Mwenyezi Mungu kwa mnyama huyu ambaye Mwenyezi Mungu amekumilikisha? Kwani mnyama huyu amenishitakia kuwa unamuweka njaa na kumtesa kwa kazi nyingi***".

Ni namna gani wanadamu wote wanavyohitajika kujipamba na maadili ya Qurani Tukufu, Kitabu cha rehema usalama na amani.

Ninakamilisha hutuba kwa maneno mawili, la kwanza ni kwa watu wa Qurani, na lengine ni kwa wasomi duniani, tunasema kwa watu wa Qurani: Ipambeni vizuri Qurani kwa sauti zenu na isikilizisheni dunia yote, enye watu wa Qurani ipambeni Qurani kwa tabia zenu njema, na ifanyeni majibu yenu kwa watu wajinga, ilindeni sana Qurani Tukufu kwa kuisoma na kujifunza pamoja na kuifahamu na kuifanyia kazi. Ewe Mwenyezi Mungu yeyote mwenye kutaka kukifanyia ubaya Kitabu chako basi urudishe ubaya wake shingoni mwake, na fanya mipango yake maangamizo yake, na tuoneshe ndani ya Qurani maajabu ya uwezo wako…na ifanye mazingatio kwa mwenye kuizingatia.

Tunasema kuwambia Wasomi duniani kuwa, ulimwengu hauwezi kubeba vita vya kidini na kuongezea vita vinavyoendelea, hivyo chukuweni mapendekezo na kuyatumia katika kuondoa kila aina za chuki za kidini kabla ya kupitwa na wakati, kwani misimamo mikali hupelekea kwenye siasa kali.

Bila ya shaka kuwa Waislamu wote wanawivu na dini yao kwa hakika wanakerwa kufanyiwa uadui Mtume wao au Kitabu cha Mola wao, Wasomi hata wajipambe namna gani na hekima au subira kwani utafika wakati ambao hekima hii itaisha na jambo kuondoka mikononi mwa Wasomi na wazee na kuwa fitina kama vile kipande cha usiku wa giza hakuna anayefahamu mwisho wake isipokuwa Mwenyezi Mungu.

**Ewe Mwenyezi Mungu tunufaishe na Qurani Tukufu.**